**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**KAWAWA JKT PRE AND PRIMARY ENGLISH MEDIUM SCHOOL**

**Email:kawawajktpreprimary@gmail.com**
**SIMU:0764053052/0764606964**

# MTIHANI WA ROBO MUHULA - DARASA LA TATU

**JINA ____________________________________________ DATE: MARCH 26, 2025**

**MAELEKEZO**

**MUDA: SAA 1:30**

**1. Mtihani huu una sehemu nne, yaani sehemu A, B, C, D na E.**

**2. Jibu maswali yote katika mtihani huu.**

**3. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**

**4. Uchafu wa kazi utakupotezea alama za mtihani wako.**

## SEHEMU A:

**1. Sikiliza kwa makini sentensi zizosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoandaliwa.**

i. ____________________________________________________________

ii. ____________________________________________________________

iii. ____________________________________________________________

iv. ____________________________________________________________

v. ____________________________________________________________

## SEHEMU B: MATUMIZI YA LUGHA

**2. Chagua herufi ya jibu sahihi kisha jaza katika kisanduku kilichoandaliwa.**

i. Neno **tikitimaji** lina silabi ngapi? ____________

(a) 3 (b) 4 (c) 5 (d) 2 ☐

ii. Neno lipi ni tofauti na maneno mengine katika haya yafuatayo? ______

(a) Macho (b) kiatu (c) mguu (d) mikono ☐

iii. "Usiache mbachao kwa msaala upitao". Sentensi hii ipo katika wakati gani?

(a) uliopita (b) ujao (c) uliopo (d) mtimilifu ☐

iv. Mchwa, nyuki, buibui, inzi kwa pamoja huitwa__________

(a) Wachafu (b) wadudu (c) wabaya (d) chakula ☐

v. Neno lenye maana sawa na neno **suluhisha** ni ______.

(a) patanisha (b) gombanisha (c) furahisha (d) uadui ☐

## SEHEMU C: LUGHA YA KIFASIHI.

3**. Jibu maswali haya**

i. Mgaa gaa na upwa? ________________________________

ii. Jungu kuu, __________________________________

iii. Ndo ndo ndo _____________________________________

iv. Nini maana ya nahau **kuanua matanga? ______________________________**

v. Hulala tulalapo huamka tuamkapo __________________________________

vi. Hasimamishwi akiwa na ghadhabu____________________________________

vii. Kuanua matanga, nini maana ya nahau hii __________________________

viii. Kila niendapo ananifuata ___________________________________

## SEHEMU D: UTUNGAJI

**4. TUMIA MANENO YAFUATAYO KUKAMILISHA HABARI HII**

| **Kunywa, safi, salama, uhai, mifugo, viumbe hai** |
|---|

Maji ni muhimu sana katika maisha ya (i) ______________________________ Mahali pasipo na maji ya kutosha huhatarisha (ii) ________________________ Wafugaji wengi huteseka kulisha na kunywesha (iii) ________________________ yao katika kipindi cha kiangazi. Umuhimu wa maji ni mkubwa kwa maisha ya binadamu, hasa kufua, kupikia (iv) __________________ na kuoga. Watu wa afya wanashauri kunywa maji safi na (v) ________________________________.

**5. Panga maneno yafuatayo kwa kuzingatia alfabeti za kiswahili**

i. Changarawe, Zabibu, Ukwaju, Katapera

____________________________________________________

ii. Abigaeli, Kaka, Kalamu, kiatu

______________________________________________________

iii. Simu, Swaiba, Suzana, Subiri.

_______________________________________________________

iv. Meza, Dawati, Kiazi, Bilauli.

_______________________________________________________

v. Chungwa, Andazi, Pilau, kuku.

_______________________________________________________

**SEHEMU E: UFAHAMU**

**6. Soma kifungu hiki cha habari kasha jibu maswali.**

Baada ya kushindwa maisha ya mjini Sara na mumewe walirudi kijijini kwao Mandepwende. Walistaajabishwa na unafuu wa maisha ya kijiji chao. Gharama za chakula zilipungua mara dufu, kila kitu kilipatikana . Waligundua mjini si chochote ni usumbufu tu. Watu wengi wana fikra za zamani ya kwamba vijijini huduma ni duni, la hasha! Tofauti na zamani nasi tuna umeme, shule zimejengwa, barabara za lami hadi mlangoni na usafiri hadi barazani. Hivyo hakuna tofauti kati ya maisha ya kijijini na mjini siku hizi.

**MASWALI**

i. Habari hii inamuhusu______________________________________________

ii . Sara na mumewe walistaajabu kitu gani baada ya kufika kijijii?

______________________________________________________________

iii. Kijiji cha kina Sara kinaitwa ________________________________________

iv. Gharama za chakula zilipungua mara ngapi? ______________________________

v. Kuna tofauti kati ya maisha ya kijijini na mjini siku hizi?

______________________________________________________________

**IMLA**

**1. Likizo moja tukiwa safarini.**

**2. Nilikua mimi, mama, baba na kaka.**

**3. Tulifika sehemu ya kula chakula.**

**4. Niliagiza nyama, ndizi na soda.**

**5. Ghafla, nikajikwaa na kuanguka puuh!**